

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA MKUU WA WILAYA KISARAWA**



# **TANGAZO**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kisarawe inawatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Kisarawe kuwa kutakua na zoezi la usaili wa vijana wanaotaka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa hiari kwa mwaka 2022/2023.

Maombi yote yapitishwe kwa Mtendaji wako wa Kata na yawasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kisarawe kwa anuani S.L.P 28003.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 5/9/2022, baada ya tarehe hiyo maombi hayatapokelewa. Kwa watakaochaguliwa usaili utafanyika tarehe 6/9/2022 katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kisarawe.

**Zifuatazo ni sifa za kuzingatia  
katika zoezi la kuwaandikisha vijana**

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Umri.
  - a. Kwa vijana wenye elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18.
  - b. Vijana wenye elimu Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka 20.
  - c. Vijana wenye elimu Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22.
  - d. Vijana wenye elimu ya stahada umri usiwe zaidi ya miaka 25.
  - e. Vijana wenye elimu ya shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26
  - f. Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 30.
  - g. Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamivu umri usiwe zaidi ya miaka 35.
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yeyote ya michoro mwilini (Tattoo).
4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari kidato cha nne na cha sita wawe waliomaliza kuanzia mwaka 2019, 2020, 2021 na 2022 wenye ufaulu ufuatao:-

- a. Wawe wamefaulu na wawe na alama (Points) zisizopungua 32.
  - b. Vijana Kidato cha Sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne.
6. Awe na elimu ya msingi aliyehitimu darasa la saba.
  7. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
  8. Awe na cheti halisi cha kumaliza shule (School Leaving Certificate).
  9. Awe na cheti halisi cha matokeo (Original Academic Certificate/Transcript).
  10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au KMKM wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.
  11. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma.
  12. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
  13. Kwa wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na sanaa sifa za elimu ni sawa na zilizotajwa hapo juu.